# Karibu kwenye **InfCareHIV**

### InfCareHIV ni nini?

Katika InfCareHIV kuna taarifa za zaidi ya 99% ya watu wote wanaoishi na virusi vya ukimwi inayojulikana nchini Sweden. InfCareHIV hufanya kazi kwa njia ambayo madaktari na wauguzi katika kliniki za virusi vya ukimwi hu andikisha taarifa wakati unapojisajili kwenye kliniki na pia wakati wa ziara za ufuatiliaji. Taarifa hizi hutumika: kusaidia wewe na daktari wako **kufanya maamuzi** na **kuboresha ubora** wa huduma za virusi vya ukimwi hapa nchini Uswidi.

### Taarifa zinazokusanywa

Tunakusanya taarifa muhimu kwa ajili ya **kufuatilia afya yako** na **ubora wa huduma za afya.** Taarifa kadha hupatikana kwa kuzungumza na wewe kama muuguzi, (kwa mfano: jinsia uliyozaliwa nayo, utambulisho wa kijinsia, nchi ya kuzaliwa njia uliweza ya kupata virusi vya ukimwi), Taarifa nyingine hupatikana kutoka kwenye rekodi za hospitali, kama: (majibu ya vipimo, matibabu ya sasa na ya zamani ya virusi vya ukimwi na magonjwa mengine. Pia tunaandika maoni yako kuhusu afya yako na huduma unayopata kwa kliniki yako ya virusi vya ukimwi kwa kupitia dodoso za afya.

### Jukumu Yetu

Tunahakikisha kwamba taarifa zako katika InfCareHIV zinalindwa. Taarifa zako katika rejista ya ubora zinaruhusiwa kutumiwa tu ili kuboresha na kuhakikisha ubora wa huduma za afya kwa watu wenye HIV na kwa ajili ya uchunguzi. Kama taarifa zinatolewa, zinakuwa zimefichwa utambulisho wako (mpokeaji hawezi kujua ni wewe). Kama taarifa zinahitaji kutolewa, lazima kwanza kufanywe ukaguzi wa usiri (kuhakikisha kwamba huwezi kuathirika kwa kutolewa kwa taarifa hizo). Uchunguzi wote lazima kwanza ukubaliwe na mamlaka ya Etikprövningsmyndigheten.

### Haki Zako

Una haki kila wakati ya kukataa kushiriki, kuacha ushiriki wako katika rejista ya ubora na kufuta taarifa zilizowekwa hapo zamani. Pia una haki ya kujua ni taarifa gani zimeandikwa kuhusu wewe na kurekebisha taarifa ambazo si sahihi au hazijakamilika. Katika hali hiyo, wasiliana na mhudumu wako wa afya. Unaweza kusoma zaidi kuhusu haki zako katika Taarifa za mgonjwa (Patientinformationen) kwenye infcarehiv.se.

### Unachangia kuboresha huduma ya afya

Kwa kushiriki katika InfCareHIV, unasaidia kuboresha huduma za afya kwa watu wenye virusi vya ukimwi. Kushiriki katika InfCareHIV ni kwa hiari na hai athiri huduma ya afya unayopata. Taarifa hutumiwa kulinganisha huduma za afya kati ya hospitali na wanaotoa huduma mbalimbali nchini yote. Baadaye, matokeo hutumiwa katika kazi ya kuboresha huduma.

### Utafiti

Watafiti hutumia taarifa zisizo na majina kutoka InfCareHIV ili waweze kuelewa huduma za virusi vya ukimwi, kuboresha matibabu na kujua hatari ya kupata magonjwa mengine ukiwa na virusi vya ukimwi. Utafiti huu husaidia kuongeza maarifa na kuboresha huduma za afya ya ugonjwa wa virusi vya ukimwi.

### Sheria na Kanuni

Maelezo zaidi yanapatikana katika (Patientinformationen) kwenye infcarehiv.se. Unaweza pia kusoma zaidi kuhusu rejista za ubora kwenye kunskapsstyrningvard.se. Kama unataka barua kwa mkono ya taarifa za mgonjwa, unaweza kuwasiliana na mhudumu wako wa afya. Utunzaji wa taarifa katika InfCareHIV unasimamiwa na sheria ya ulinzi wa taarifa (dataskyddsförordningen), sheria ya taarifa za wagonjwa (patientdatalagen) na sheria ya usiri na taarifa za umma (offentlighets och sekretesslagen). Mamlaka kuu inayosimamia taarifa ni hospitali ya Karolinska huko Stockholm (Karolinska Universitetssjukhuset) Mhudumu wako wa afya ndiye mwenye jukumu la kushughulikia taarifa zako wakati taarifa kuhusu wewe zinakusanywa kwa ajili ya InfCareHIV.

InfCareHIV Kvalitetsregistret
för personer med hiv